Kadhi Mkuu wa Kenya aiombea serikali amani na ufanisi

ALHAMDU lillah, kwa kuipokea tena Siku Kuu ya Idd el Haji kwa salama na amani katika nchi yetu ya Kenya. Hatuna budi katika wakati huu wa furaha na sherehe kwa ajili ya kuadhimisha Siku hii Kubwa, kuiombea dua Serikali yetu tukufu ikiongozwa na Kiongozi mpendwa Bwana Daniel Arap Moi.

Huu ni wakati wa Waislamu kuomba dua nyingi nyingi ili Kenya idumishe amani, ufanisi na upendo. Waislamu popote pale walipo na hasa wale ambao mwaka huu wamekuwa wahijaji kutoka Kenya, waiombee nchi yetu ya Kenya Mwenyezi Mungu ainusuru na fitina za kutoka nje. Mungu ainusuru Kenya na balaa za maradhi njaa na fitina. Mungu awasaidie viongozi wetu kuiongoza nchi hii kwa salama na amani.

Kwa niaba yangu mimi mwenyewe, nawapeleke salamu za Idd Waislamu kote nchini Kenya. Na nawaomba Waislamu waishi kwa salama na amani katika miji yao na waisaidie Serikali yetu kuondosha balaa zote na kila aina ya uchochezi toka kwa maadui zetu. Nawaomba Waislamu wawe watulivu na wao wenyewe wasimame msimamo mmoja katika kuendesha mbele mambo yao ya kidini.

Nawahimiza Waislamu katika Siku Kuu hii wanyooshe mikono yao ya ukarimu kwa ndugu zao wa Kiislamu ambao pengine hawakubahatika sana kama wao ili na wao siku hiyo wale chakula kizuri na wawavishe watoto wao nguo nzuri kama watoto wengine. Angalieni sana siku hiyo watoto mayatima, majirani zenu, watu wazima wasiojiweza. Almuradi kila Mwislamu siku hii msaidieni kwa chakula ama kwa matumizi ili furaha iwe kwa wote.

Mwenyezi Mungu mtawilishe umuri Rais wetu mpendwa pamoja na aila yake. Uwatie nguvu Mawaziri na Wabunge na Madiwani ili watekeleze kazi zao za kuhudumia raia bila ya tabu yoyote. Mungu tudumishie amani, raha na starehe katika nchi yetu na ulimwenguni kote.

Idd Mbarak.

Abdalla Saleh El Farsy,
Kadhi Mkuu, Kenya.

WATOTO WALIO jaa furaha tele wakiwa wamevalia maridadi tayari kwa sherehe za Idd-ul-Haj. Kutakuwa na michezo ya aina mbali mbali kuwafurahisha watoto kama hawa katika maonyesho ya Makadara.

PICHA: HUMPHREY MUMIA



SHERIA YA Kiislamu imeamrisha kwamba waumini wanaposali waelekee Kibla ambako ndiki iliko Al-Kaaba. Sasa vipi mtu ataweza kutambua Kibla kama yuko nchi za Ulaya? Kampuni moja nchini Austria inayoitwa Benko Ing. Kornhuber imeunda Dira ambayo inamwezesha muumini wa Ulaya kutambua Kibla bila ya shida yoyote. Dira hiyo kama inavyoonekana pichani, ina orodha ya majina ya miji kadha na wakati ncha ya Dira hiyo inapoelekezwa Kaskazini, basi ncha ya pili huelekea Makka.

PICHA: MEETCH BAKHRESA

SHIRAZY AWAOMBEA WAHIJAJI WOTE HIJA YA KHERI NA FURAHA

HAYA ndio majira ya Waislamu kuzidi kukumbushana yale mafunzo yao ya Kujitolea kwani wakati wa kuhiji Maka na Kuzuru Madina Waislamu hujitolea hali na mali yao kutekeleza mwito wa Mola wao, kuthibitisha imani yao.

Wale walio na bahati ya kwenda kutekeleza nguzo ya tano ya Uislamu — Haj — huingiwa na imani na kujihisi kwamba Mungu amewatunuku jambo kubwa la kuweza kufika Meka na kufanya mambo yote wanaotakiwa wayafanye hiyo ibada ya Haj. Waislamu waliobaki makwao huwa wakiwaombea Mungu ndugu zao na dada zao na pia Waislamu wote watakabaliwe ibada zao zote za Haj.

Nami kwa niaba ya Thalatha Twaifa, nachukua nafasi hii kunjufu niwaombee ndugu zetu wote Waislamu waliokwenda Maka wafaulu katika ibada zao na warudi nyumbani kwa furaha na salama.

Pia nachukua fursa hii kumuombea Mungu kwa unyenyekevu, Mtukufu Rais Daniel Arap Moi kwa kujitolea maisha yake na wakati wake wa thamani kwa kutumikia umma wake wa Kenya na Bara zima la Afrika kwani katika safari zake za huko Amerika na Australia amedhihirisha wazi kwa ulimwengu mzima kwamba nia yake thabiti ni kuliona Bara zima la Afrika liko huru katika amani na maendeleo.

Twamshukuru Mola wetu kutupatia kiongozi huyu Rais wetu mpendwa Moi, Mungu amzidishie hekima, ghera na uwezo wa kuwatumikia watu wake wote na umma wa Bara zima la Afrika.

Idd Mubaraka.

Mohamed Salim Shirazy,
Tamimu wa Thalatha Twaifa.

COASTWEEK YATOA MKONO WA IDD KWA WASOMAJI WOTE WA KIISLAMU

WAKATI MWENGINE wa kusherehekea Siku Kuu ya Idd umefika. Na mara hii, ni Idd el Hajj. Hii ndiyo Siku Kuu kubwa kwa Waislamu. Ina mafunzo tele kwa Waislamu. Kwanza inatukumbusha mambo ya Hijja na vile hasa yalivyoanza. Kwa hivyo inatoa nafasi ya kumkumbuka Naby Ibrahim na mtoto wake Ismail. Tena inatukumbusha malezi na utii wa wana kwa baba zao. Kwani tukumbuke kwamba Nabii Ibrahim alipooteshwa kumchinja mwanawe, hakusita. Na huyo mwana naye alipopawa khabari na babake kwamba ameamriwa amchinje, hakukimbia wala kuwazawaza, bali alimwambia babake, "fanya kama ulivyoamriwa nami utanikuta ni wenye kusubiri."

Hayo ndiyo malezi. Jee Waislamu wanaitumia nafasi hiyo kwa kuwalea watoto wao ipasavyo? Lakini Mwenyezi Mungu alikuwa tu akiipima amri ya mtume wake Ibrahim. Na Mola alipotosheka na utii wa baba na mwanawe, alimletea mnyama kutoka mbinguni (dhabhi) amchinje badili ya mtoto wake. Na kwa kukumbuka tendo hilo la imani kubwa na utii mkubwa hadi leo Waislamu wanafanya tendo hili la kuchinja mnyama kila ifikapo Idd el Hajji.

Ni watoto wangapi leo wanaotii baba zao. Baba anamwambia mtoto wake mwanangu usende pahala fulani kwani utaharibu Uislamu wako na utaharibu imani yako. Lakini wapi? Mtoto asema mzee wewe yako yamekwishia, "hapo zamani pia wewe ulikuwa kijana kama mimi lakini leo unkwishiwa ndipo wataka na mimi nijiweke makazi yako."

SOTE TUWE MAKARIMU

Waislamu wenye tabia ya kuadhimisha Idd el Hajji kama ipasavyo, bila shaka hawatakosa baraka za Mungu na amani yake kama vile alivyozipata Naby Ibrahim. Siku hiyo, ukarimu unataka uwe ule wa hali ya juu kabisa. Yaani uwe na hakika kwamba jirani yako iwapo ni maskini siku hiyo ya Idd atakula chakula kama chako pamoja na watoto wake. Uhakikishe kwamba maskini waliokuzunguka na wao siku hiyo wanapata chakula bila ya kusumbuka. Kwa nini tendo hili la ukarimu tuwaachie ndugu zetu wa Kihindi peke yake, na ilhali amri hii yote yatuhusu?

Mwaka huu, Idd el Hajji imekuja siku ya Ijumaa, siku tukufu kwa Waislamu. Sasa hatujui mpaka sasa kwamba Sala ya Ijumaa pia siku hiyo itasaliwa. Asili ya kusema hivi ni kwamba iwapo sala ya Idd imetokea siku ya Ijumaa basi sala ya Idd hutoshea na baadaye pakasaliwa tu sala ya kawaida ya adhuhuri, maana huwa Waislamu wa mji mzima wameshakutana na kwa hivyo hakuna haja ya kukutana tena wote mara ya pili. Kitu muhimu zaidi ni Waislamu kuja pamoja na kusameheana na pia kuzidi kuomba Mungu wawe kitu kimoja katika mambo yao ya Kidini. Pasiwe na utengano kati ya Waislamu. Neno lao liwe moja tu.

Na kwa niaba ya Wahariri wenzangu wa *COASTWEEK* twawapelekea wasomaji wetu mkono wa Idd-el-Hajji popote pale ambapo gazeti hili husomwa. Na twawambia hivi: "Kulla aam wa antum bilkheyr".

Iddi Mbarak.

KWA HAKIKA KWELI YAUMA

YAONESHA Bibi Zaitun Said Mohamed anaielewa Tafsiri ya Quran tukufu sawa sawa pamoja na Biblia.

Kabla sijajibu suala zake alizouliza (*COASTWEEK* 2.10.81) ningelipenda anijibu hizi suala zangu ndogo kwanza. Pengine tafsiri ya Quran aliyonayo Zaitun maeleza vizuri kuliko Tafsiri aliyonayo mimi.

• Aya gani katika Quran inataja kwa majina kuwa Vodka, Matingasi, Champagne, Chang'aa, Johnny Walker, Martel Cognac ni haramu?

• Aya gani katika Quran inatwambia kanzu, kikoi na kofia ni vazi la Ki-Islamu?

• Aya gani katika Quran inasema gari ni uzushi mbaya?

Nguo za heshima ulizotaja katika barua yako ambazo wanawake wanavaa hadhari ni zipi?

• Mwanamume ambae hendi Kenyatta Hall kumtukuwa mke wake huwa yeye hajulikani kama ni mume wa fulani?

Idd Mubarak.

Mdadisi Bint Maskini,
Biyams Road, MOMBASA.

SAUTI ZA WASOMAJI

COASTWEEK Sanduku La Posta 87270, Mombasa KENYA

WALILIA VIPANDE VYA KANU TAITA

TUNAYO offisi ya KANU mjini Taita lakini tatizo ni kwamba katika afisi hiyo haina Mwenyekiti wala Mweka Hazina kwani ufikapo hapo offisini utakuta tu walinzi na wafyagiaji.

Nasi watu wengi wa Taita twataka zote tuwe na Kadi za uwanachama wa KANU, lakini pakupata hizo Kadi Wilayani kwetu ndio zii!!

Tuchague Viongozi

Kwa hivyo naomba Wabunge wetu wa Taita waitishe mkutano ili tuchaguwe Mwenyekiti, Mweka Hazina, na wengineo ili afisi yetu tuifutue upya kabisa, kwani walioko sasa hawana lolote watutendealo.

Munyika Mwaigho,
Magongo, MOMBASA.

JISHINDIE
Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza ...no

SWAHILI CROSSWORD NO.



JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

KWENDA KULIA:

1. Msimamizi wa wafanyi kazi za mikono
5. South Afrika
6. Mwenziwe pishi
7. Huwa katika shaza baharini
9. Osha, safisha
11. Nyama nyekundu tumboni
14. Shutumu, aili
15. Nusu ya neno nini
16. Neno la kukataa
17. Panda, kwea

KWENDA CHINI:

1. Stesheni kati ya Mombasa na Nairobi
2. Mpaka
3. Mwanzo
4. Tamu kushinda sukari
8. Teketeza
10. Chakula mashuhuri
12. Toa mazao
13. Toa kilicho mdomoni
15. Kiungo cha maneno.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 127

1] Julius D. Katana, Sanduku la Posta 25, Kaloleni, Giriama.

2] Mr. M. K. Kumenzwa, Sanduku la Posta 80149, Msa.

3] Mohamad Hemed, Sanduku la Posta 68, Lamu.

Washindi waombwa waike afisini mwa *COASTWEEK*.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 127—

KWENDA KULIA:

1. COASTWEEK, 4. ASIHI, 6. MKOA, 7. AKILI, 9. NI, 11. VUMBA, 13. BIRIKA, 14. KAA 15. AU, 16. JA.

KWENDA CHINI:

1. CHAPATI, 2. SAHALI, 3. EZEKA, 5. TANGAZA, 8. INDIA, 10. KUKU, 11. VIA, 12. MA, 13. BA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayo-kubaliwa.

Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LIMITED*, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano terehe 21.10.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.